# Learning by Ear – Religious Dialogue: "A Bridge over Gori"

## Episode 02: "Niko nilivyo kwasababu yako"

**Author: Romie Singh**

**Editors: Katrin Ogunsade, Naïma Guira**

**Proof reading: Natalie Glanville-Wallis**

**Expert on African religions: Jean-Félix Belinga Belinga**

**KiSUAHELI ERIC PONDA**

**List of characters for episode 2:**

- Narrator /Philip male (17)
- Harry, male (17)
- Mat, male (16)
- Layla, female (16)
- School director, Mrs. Ayo Milulu, female (48)
- Father Barnabus Dembele, Harry´s uncle (49)
- Hassan, Layla´s brother (12)
- Philip´s father, Layton-Browne (50)
- + Student chatter
- + Students and teachers (singing anthem)

- <u>+ Students and teachers (saying prayer)</u>

1. **<u>SIG TUNE UP</u>**

2. **<u>INTRO:</u>**

**Hujambo na karibu kwa kwa sehemu ya Pili ya mchezo huu wa Radio wa *DARAJA LA GORI,* Hadithi inavyoelezea jinsi Dini na Siasa zinavyoweza kusababisha mtafaruku baina ya Jamii na , Familia mbili, na hali kadhalika kwa wapenzi wawili Harry na Layla.**

**Ni mwanzo wa mwaka shuleni Ubuntu. Philip, ni mmoja wa Marafiki wakubwa wa Harry.Yeye ndiye atakayekusimulia makala hii kwa jina"Niko nilivyo kwasababu yako". Katika sehemu hii Philip anajikuta na kishindo kikubwa shuleni na kwa upande mwengine anashinikizwa na Babake.Layla na Harry nao wanakumbana na vikwazo nyumbani. Endelea kuwa nasi!**

**<u>Scene 1. In school assembly hall</u>**

**Director, Students, Harry, Mat, Philip, Philip Narrator**

3. **<u>SFX: In a big hall. Student chatter. Noise slowly dies down as director speaks</u>**

4. **DIRECTOR:** **Habari za asubuhi na karibuni tena hapa shuleni Ubuntu. *(Noise dies down)* Kwa wale ambao ni wageni shuleni humu, nachukua fursa hii kujitambulisha. Mimi ni ndie mkurugenzi wa chuo hiki na jina langu ni Ayo Milulu. Shule yetu imekuwako kwa**

**miaka 10 sasa. Ubuntu ni nembo inayoashiria malengo ya shule hii. Na Maana yake ni "Niko nilivyo kwasababu ya ulivyo" Ni sehemu ya mila na tamaduni za Kiafrika.**

***FADE UNDER AND OVER PLAY THE FOLLOWING CONVERSATION***

***Bila ya jamii, sisi tu wadhaifu na wapweke. Jamii yetu ni Familia yetu,shule yetu ,na hata majirani wetu ndio nguzo inayotupa msukumo wa yale yote tufanyayo.Ni kwasababu ya uhusiano huo ndio tunaimarika.**

5. **HARRY:** ***(whispering)*** **Hebu jaribu kumweleza Baba Mdogo hayo! Anadhani yeye ni mwakilishi wa Mungu hapa Duniani..!.**

6. **PHILIP:** ***(whispering)*** **Ai! Harry! Babako mdogo ni kasisi mzuri sasa..!.**

7. **HARRY:** ***(whispering)*** **Kwanini unamuunga mkono Philip? Heee..ananiharibia kwa kunishinikiza mimi pia niwe kasisi wa kanisa katoliki!**

8. **DIRECTOR:** ***(Louder)*** **Tusimame sote kwa wimbo wa Chuo chetu!**

9. **Song: Ubuntu Anthem**

**10. NARRATOR/PHILIP: Ubuntu kilikuwa chuo maalum. Wanafunzi walihitimu baada ya miaka miwili tu, lakini katika muda huo, tulijifunza mengi kuhusu tamaduni na imani za kila mmoja wetu.Ama kwa hakika tulikuwa wakazi wa eneo moja, lakini hatukufahamu chochote kuhusu dini za wenzetu.Wengi wetu walidhani wanajua kila kila kitu, na mara nyingi walijikuta kwamba hakuna wanalolijua, ila tu upuzi mtupu wa kuamini sana umbea, habari za Televisheni au hata filamu. Hivyo dhamira ya Shule hii ya Ubuntu ilikuwa kutuleta pamoja na kuweka bayana hali halisi,kwa lengo la kuimarisha uhusiano,uvumilivu na kuheshimiana.**

**11. *LEARNERS AND TEACHERS START SOFTLY SPOKEN PRAYER (see below)***

***FADE UNDER PHILIP AND UP AGAIN***

**12. ALL** ***Ewe mwenyezi Mungu tupe amani ya kweli na yenye kudumu,ili mioyo yetu pia iweze kuieneza amani hiyo.***
***Mwenyezi Mungu tupe amani,na hekima ili tuwe na vitendo,fikra na kauli njema.***

**FADE OUT. BRING UP PHILIP**

***Ewe mwenyezi mungu, tupe amani, ili nasi tuweze kutosheka na kukutolea shukrani kwa yote mazuri.***
***Mwenyezi mungu tupe amani tuweze kuzifurahia neema zako licha ya majaribu ya ulimwengu.***
***Ewe Mungu tupe amani ya kudumu na kustahamili yote kwa neema na huruma zako.***
***Mwenyezi mungu tupe amani ili mioyo yetu iweze kuuona utukufuwako na kuondoa kiza kilio mbele yetu..***

**13. PHILIP/NARRATOR:** **Kila asubuhi tuliianza siku kwa maombi yasiyojikita kwenye madhehebu yoyote,bali sala ya kumtukuza Mwenyezi Mungu inayokubalika na wote hata kama mimi ambaye sikuwa mfuasi wa madhehebu yoyote.**

**14. DIRECTOR:** *(End of prayer)* ***Mwenyezi Mungu tupe amani,ewe Bwana baba zetu na Mama zetu, ili sie wanao hapa ulimwenguni tuweze kuishi pamoja kwa amani kama familia moja Amen…...***

15. ***SFX: Rustle as learners cough and move***

16. **DIRECTOR:** **Kwa kuifuata misingi iliyowekwa na muasisi wa chuo hiki,Chifu Solomon Banda, nachukua fursa hii kuwatangazia majina ya kiranja wa kike na Kiume hapa shuleni. Hawa watakuwa wawakilishi wenu na kiungo baina yangu na nyinyi wanafunzi.. Nao ni *(pause):* Layla Omer na Harry Dembele**!

17. ***SFX: Excited murmur among the learners***

18. **DIRECTOR:** **Tafadhali njooni hapa mbele mchukue vibandiko vyenu.**

19. **MAT:** ***(Whisper)* Philip lazima uwe umevunjika moyo sana! Nilidhani wewe ni chaguo la moja kwa moja kwa wadhifa huu!**

20. **PHILIP:** ***(Whisper)* Ahsante Mat, lakini nadhani ni kwasababu Babangu si Kasisi na mtu mwenye ushawishi mkubwa katika jamii!**

21. **MAT:** ***(Encouraging)* Tafadhali usiliruhusu hili liwe kikwazo katika uhusiano wako na Harry, kumbuka sisi bado ni madume wa shule hii ya Ubuntu sivyo?**

22. **PHILIP:** ***(sounding deflated)* Ni kweli!**

23. **APPLAUSE. FADE**

**24. PHILIP/NARRATOR:** **Ghafla niliingiwa na baridi, kwasababu nilijua nafasi hiyo ilikuwa yangu.Umri wangu uliuzidi ule wa Harry, na kisha nilikuwa nimepata alama nzuri zaidi kuliko Harry. Kwanini hawakuyazingatia yote haya. Pia Babangu hakufurahishwa kamwe na taarifa hizo.**

**<u>Scene 2. At the Layton-Browne's</u>**

**Philip's father (Layton Browne), Philip**

**25. <u>SFX: Radio / Music on in the background</u>**

**26. P's FATHER:** ***(Irritated)*** **Lakini nadhani nilimfahamisha wazi wazi mwalimu mkuu, Philip!. Kwamba ni muhimu kujumuisha watu kama sisi walio na mitazamo tofauti na wenye shauku kuhusu habari za mungu. Sisi huwa tunapinga madai yanayotolewa na baadhi ya watu kwamba kuna mungu mmoja, na huwa tunatoa mwelekeo wa uongozi usiojikita kwenye dini. Hayo ndio taifa hili linayohitaji!**

**27. PHILIP:** **Oh Baba, mbona hukumshawishi Bibi Milulu. Kumbe ndio sababu hakunichagua kuwa kiranja wa wanafunzi Shuleni.**

**28. P'FATHER:** **Upuzi mtupu! ….Sawa! …Na kwanza hebu niambie, nani amechaguliwa kiranja kwa upande wa wasichanal?**

**29. PHILIP:** ***(embarrassed)*** **Hmmm, ni Layla Omer.**

**30. P's FATHER:** ***(very interested)*** **Kweli!** ***(warmly)*** **Layla? Hmmm,** ***(coming out of his thoughts)*** **Ehhhh.. ndio … hiyo ni sawa kabisa. Binti yule.Sasa ameondoa haya. Na kwanini unanitazama hivyo?** ***(Anxious)*** **Nataraji huna hisia za kuwa na uhusiano na yeye..?*****.(Heated)*** **Mungu wangu, haiwezekani….huwezi….ehh…ehh…..**

**30. PHILIP:** *(heated)* **Kwanini ?Au kwasababu ni Muislamu? Sasa kwanini ukanipeleka shule hii ya Ubuntu ilhali hutaki tutangamane!**

**31.** ***FADE MUSIC. CHANGE IN PHIIP'S VOICE TO NARRATOR***

**32. PHILIP/NARRATOR: Babangu alitoka chumbani kwa hasira! Nilibaki nikijiuliza kilichomkasirisha? Wakati huo huo Layla naye alikuwa anakabiliwa na kivumbi chake tu kutoka kwa mdogo wake ambaye hajaifurahia hatua ya yeye kuteuliwa kuwa kiranja wa wasichana!**

**Scene3. At the Omer's**

**Hassan, Layla**

**33.** ***Islamic religious music in the background***

**34. HASSAN: Layla, kwanini Chuo chenu kinahitaji kiranja wa kiume na wa kike?**

**35. LAYLA: Ili masuala yetu yashughulikiwe pia Hassan. Wanawake wana haki zao, na hii ndio sababu kubwa!**

**36. HASSAN: Lakini ni Wanaume ndio viongozi, sio nyinyi wasichana … nyinyi mtaolewa na kuwa walezi wa familia…Huku ni kupoteza wakati tu…. Kumsomesha msichana ni kupoteza wakati!**

**37. LAYLA:** ***(angry)*** **Wewe ndie unayenipotezea muda wangu.. Naenda kufanya mazoezi..!.**

**38. HASSAN:** **Huwezi…., Msichana wa kiislamu hapaswi kuuonyesha uso wake hadharani!**

**39. LAYLA:** ***(quietly)*** **Hassan, nitavaa hijab….Ninachohitaji ni kufunika uso wangu…!Sijui munafunzwa nini katika chuo cha Madrasaa, lakini Msichana wa kiislamu anaweza kutoka nje na kushiriki katika michezo ilmradi awe amejistiri. Hata Mtume Mohammad" (rehma na amani zimfikie), aliyasema hayo!**

**40. HASSAN:** **Msichana wa Kiislamu hapaswi kuuonyesha mwili wake kwa wasio wa imani hiyo.Usidhani kwavile Baba hayupo hapa nyumbani unafikiri unaweza…….**

**41. LAYLA:** **Baba anazifahamu sera za shule yetu. Kama hilo linakutatiza, basi nenda ukazungumze na mkurugenzi mkuu Bi Milulu.Lakini mimi nitafanya yale niliyoruhisiwa kufanya na waalimu.**

**42. *SFX: jumping up from chair, running out, slams door***

**43. HASSAN:** *(off mic)* **Hebu subiri …nitaandamana na wewe…!.**

**44. BRIDGING MUSIC UP**

**45. PHILIP/NARRATOR: Kwa upande mwengine Harry alikuwa na furaha isiyo na kifani,Kiranja wa kiume! Mtoto wa Chifu na mpwa wa Kasisi Barnabus, kiongozi mwenye ushawishi mkubwa miongoni mwa jamii ya Kikatoliki ya Gori. Hata hivyo askofu Baba Mdogo kamwe hakufurahishwa na aliyokuwa akifanya Mpwawe!**

**Scene 4. At Father Barnabus'**

**Philip Narrator, Father Barnabus, Harry**

**46. SFX: Dance music in the background**

**47. FATHER B: Punguza sauti Harry! Kwanini unapenda kucheza muziki kwa sauti ya juu?Unasahau mimi ni mtumishi wa mungu?. Hebu fanya adabu!**

**TURNS MUSIC SOFTER**

**48. HARRY:** **Samahani Baba Mdogo. Umm… Mat na Philip wamenialika tukasherehekee uteuzi wangu wa kiranja wa kiume shuleni mwetu. Ni sawa Baba mdogo?.**

**49. FATHER B:** **Harry.Kwani unataka kuwa nje muda wote? Nataka ukae humu ndani na uyape umuhimu masomo yako ya Biblia. Tunahitaji kukuandaa kuwa mtu mzima na pengine hata kuwa kasisi!**

**50. HARRY:** ***(quietly)*** **Baba Mdogo- sidhani kama mimi nitaweza kuwa kasisi!**

**51. FATHER B:** **Nyamaza-..! wewe ni kijana mdogo sana huwezi kujiamulia hilo kwa sasa.** ***(softly)*** **Hii ndio sababu niko hapa kijana wangu: kukuongoza kwa Mwenyezi Mungu..!**

**52. HARRY:** **Hmmm. Baba mdogo, leo ni Ijumaa, na nimeteuliwa kuwa kiranja. Kundi letu la madume wa Ubuntu wanataka kusherehekea….!**

**53. FATHER B:** ***(confused, stuttering)*** **Kundi gani…? tangu lini….?**

**54. HARRY:** ***(interrupting, reassuring)*** **Ni Jina tu, huwa tunacheza mpira na kufanya mazoezi pamoja……..**

**55. FATHER B:** **Na kisha kwenda Klabu pamoja?. Umepigwa marufuku kunywa pombe—kwanza wewe hujafika umri wa kufanya hayo… Na ni kiku……..**

**56. HARRY:** ***(interrupting)*** **Tunafahamu hilo Baba Mdogo, tunaenda mkahawani tu kunywa chai na juisi…na kucheza *Pool* basi!**

**57. FATHER B:** **Ufahamu tunaenda kijijini wikendi hii.Lazima tukuandae na tukuwekee sheria na muongozo mpya. Sasa unaweza kwenda!**

<u>**AMBIANCE FADE OUT**</u>

**58. PHILIP/NARRATOR: Hatimaye tunakutana mkahawani na kama desturi tunataniana na kucheka na wasichana katika mkahawa huo,kucheza *Pool* na kujadiliana .Lakini bado kuna jambo moja linalonisumbua akilini- Harry kachaguliwa kiranja wa shule pamoja na msichana mrembo Layla watakaokuwa wakishirikiana pamoja! Nilipaswa kuipata nafasi hiyo! Roho yangu ilizidi kuniuma…. Ningeacha kucheza ,mpira, na kutoka kundi la madume wa Ubuntu ili niweze kuwa na muda mwingi zaidi na yeye.Lakini haiwezekani kilichobakia ni kumtazama kwa mbali akiwa mazoezini ,au katika uwanja wa riadha huku Kakake akimfuata nyuma kila wakati.. Itanibidi nitafute njia ya kuwa karibu naye,na awe wangu.**

**59. <u>SIG TUNE UP</u>**

**60. OUTRO:**

**Na hadi hapo tunafika mwisho wa kipindi hiki cha Noa Bongo kwa leo! Marafiki hawa watatu wamefahamu, kuwa kiongozi wa shuleni sio wa nyumbani, hatahivyo kujiamini si rahisi. Ungana naye tena Harry katika makala yajayo ya mchezo huu wa Daraja la Mto Gori, upate kufahamu furaha aliyonayo ya kushirikiana na Layla, na pia anapogundua kuwa anahitaji kujitenga naye. Kumbuka ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki na vingine vingi vya Noa bongo-Jenga Maisha yako tembelea mtandao wetu wa www.dw-world.de. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa**.

**END OF EPISODE 2**